



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. JD. 236/441/01C/85

Tarehe: 04 Agosti 2023

TANGAZO LA UZAJI WA VIWANJA ENEO LA MRADI WA STENDI MPYA YA KIMATAIFA YA MABASI MAARUFU BONDENI CITY

Mkurugenzi wa Jiji la Arusha anawatangazia wananchi wote, makampuni, Taasisi za serikali na binafsi kuwa Halmashauri ya Jiji la Arusha inatarajia kuuza viwanja vilivyopangwa na kupimwa kwa ukubwa tofauti katika Kata ya Murriet, eneo maarufu kama **Bondeni City**. Katika eneo hili la mradi Serikali inatarajia kujenga Stendi ya Kimataifa ya mabasi ya Jiji la Arusha ambayo itajengwa katika mwaka wa fedha 2023/2024 na uko katika hatua ya kutafuta mjenzi. Ni eneo la kimkakati ambapo mji mkubwa wa kujitegemea (Satellite city) umeandaliwa na umezingatia Mpango Kabambe (Master Plan) wa Jiji la Arusha.

Mbali na viwanja vinavyouzwa na Halmashauri, kuna viwanja vingine vingi vya makazi, biashara, viwanda nk vinavyouzwa na Kampuni ya Bondeni Seeds Ltd ambayo ni mbia katika mradi huo. Viwanja vinavyouzwa na Kampuni hiyo vinauzwa kwa utaratibu na bei zinaowekwa na kampuni yenyewe. Wananchi wanaopenda kununua viwanja hivyo wafike katika ofisi za kampuni hiyo zilizoko katika eneo la mradi.

Viwanja vinavyouzwa na Halmashauri vinauzwa kupitia Mfumo wa ukusanyaji mapato wa Serikali unaojulikana kama TAUSI, hivyo yeyote mwenye sifa na anayehitaji kununua kiwanja kwa matumizi yaliyoainishwa afuate taratibu kuomba kiwanja kupitia Mfumo huo. Matumizi, ukubwa na bei ya viwanja vinavyouzwa na Halmashauri vinaonekana katika mfumo huo.

Tembelea Tovuti Rasmi ya <https://tausi.tamisemi.go.tz/> kisha Bofya Kitufe cha "Create Account"

Hatua ya 2: Ingiza maelezo Binafsi – NIN (Namba ya Kitambulisho cha Taifa) na nambari ya Simu ya Mkononi; kisha tengeneza Jina la Mtumiaji na Nenosiri kwa kutumia Nenosiri la Uthibitishaji wa Mlipakodi Mara Moja (OTP)

Unda Jina la mtumiaji na nenosiri la akaunti yako. Hakikisha umeziweka salama na usizishiriki na mtu yeyote.

Ukishakamilisha hatua zote Tuma maombi yako kwa kubofya kitufe cha "Submit" na kisha nenda kwenye Land Sales na jaza maelezo ya kuingia yanayohitajika; Jina la Mtumiaji (NIN) na Nenosiri. Mara tu unapokamilisha hatua zote, Bofya kitufe cha "Sign In" ili kufikia Dashibodi ya Mfumo.

Utakuwa umefika kwenye Mfumo ambapo utaona viwanja vinavyouzwa na tuma maombi yako kwa kuchagua kiwanja unachokipenda kwa kiasi cha fedha ulichonacho. Kwa maelezo zaidi juu ya ufunguzi wa Akaunti tafadhali piga simu Na. 0753 120020 au 0767 275926.

Masharti ya ununuzi wa kiwanja yanaonekana kwenye Mfumo. Tafadhali soma kwa makini na zingatia.

Andaa akaunti yako tayari kwa kuomba kiwanja na kununua kuanzia tarehe 14.08.2023 na malipo ya maombi (Tshs. 20,000) yatatakiwa kukamilishwa ndani ya siku saba (7) tangu tarehe ya kupata Control Number. Malipo ya kunua kiwanja yakamilishwe kikamilifu ndani ya muda wa siku Tisini (90) tangu kupata Nambari ya Malipo (Control Number).

Wananchi wote mnakaribishwa kuwahi fursa hii ya pekee na adimu ili kuwa miongoni mwa wananchi watakaokuwa sehemu ya Mji wa Bondenicity utakaokuwa umejitosheleza.


Dkt. Onesmo Mandike
**KAIMU MKURUGENZI WA JIJI
ARUSHA**

